



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA



MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VIFAA CHAKAVU

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa **Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)** itauza kwa njia ya mnada wa hadhara wa vifaa chakavu yakiwemo magari, samani za ofisi pamoja na vifaa vingine siku ya **Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dar es Salaam na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.**

Wananchi wote watakaoshiriki mnada huo wanaombwa kufika siku ya **Jumapili tarehe 25 Juni, 2023** katika **Jengo la UTUMISHI Kivukoni Dar es Salaam** kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo ambavyo ni viti vya ofisini **“Office Chairs”, “Printers” na “Laptops”** na siku ya **Jumanne tarehe 27 Juni, 2023** kuanzia saa **4:00 asubuhi** hadi saa **10:00 jioni** katika **Ofisi za e-GA Mji wa Serikali Mtumba Dodoma** kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo, ambapo pamoja na vifaa vingine, magari yote yameegeshwa katika **ofisi za e-GA.**

Maelezo zaidi ya magari hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali:

Na	Aina	Modeli	Namba ya Usajili	Mahali lilipo	Hali ya Gari
1	TOYOTA station wagon Diesel Engine	LAND CRUISER V8	STL2039	e-GA HQ Mtumba Dodoma	Halitembei
2	Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine,	PAJERO ST WAGON	STL2011	e-GA HQ Mtumba Dodoma	Halitembei
3	Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine	PAJERO ST WAGON	STL2010	e-GA HQ Mtumba Dodoma	Halitembei

MASHARTI YA MNADA

- Magari hayajalipiwa ushuru na kodi ya ongezeko la thamani (VAT), hivyo Mnunuzi atatakiwa kulipa ushuru na kodi zingine kabla ya kulichukua toka Mamlaka ya Serikali Mtandao
- Magari yatauzwa kama yalivyo mahali yalipo
- Mnunuzi wa gari atalazimika kulipa papo hapo amana “deposit” isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari na atakamilisha malipo yote ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi wa gari na amana iliyolipwa haitarudishwa.
- Mnunuzi wa gari atatakiwa kuondosha au kuchukua gari ndani ya muda wa siku saba (07) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
- Ruhusa ya kuangalia gari itatolewa kwa siku mbili (02) kabla ya tarehe ya mnada husika.
- Kwa Mnunuzi wa vifaa vingine atatakiwa kulipia kifaa alichopata baada tu ya kumtangaza dalali kuwa mshindi (**on fall of the hammer**). Kifaa ambacho hakijalipiwa kitanadiwa upya. Pia mnunuzi atatakiwa kuchukua kifaa alichonunua papo hapo mara tu baada ya kulipia (cash and carry)
- Mnada utaanza **saa nne (4:00) asubuhi siku ya Jumapili tarehe 27 Juni katika ofisi zake za Dar es Salaam, 2023 na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.**

Imetolewa na
Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)